BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Tatu – Tarehe 16 Februari, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

91. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na changamoto ya kupotea kwa kumbukumbu za matayarisho ya kutengenezewa vyeti vya kuzaliwa vya watoto mara kwa mara na kuwapa usumbufu wazazi kuanza kurejea zoezi hilo mara nyengine.

(a) Je, tatizo hili linasababishwa na nini.

(b) Ni lini changamoto hii itapatiwa ufumbuzi.

**Ofisi ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

71. MHESHIMIWA ZAINA ABDALLA SALUM (Nafasi za wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Naipongeza Serikali kwa kuona ipo haya ya kutowa kipaumbele kwenye mikopo kwa asilimia 2.0 kwa watu wenye ulemavu.

    Je, Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanafaidika na asilimia 2.0 ya mikopo hiyo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

97. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Kwa kiasi gani Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) linatoa mchango wa kuendeleza mila, silka na tamaduni zetu kupitia vipindi vyake mbali mbali vinavyooneshwa kwa jamii.

158. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Naishukuru Wizara yako inayoshughulikia vijana kwa kuwawezesha vijana wengi kuanza kujenga imani ya ujasiriamali na kujiajiri.

    Je, nini matarajio ya Wizara yako katika kuzalisha wabunifu mbali mbali miongoni mwa vijana, ili kuweza kufikia lengo la maendeleo makubwa katika nchi yetu.

**Wizara ya Afya:**

35. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Wanafunzi wa masomo ya afya wamekuwa wakiichagua Hospitali ya Mnazi Mmoja kama kituo chao cha kufanyia mazoezi ya vitendo ili kutimiza takwa la masomo yao kabla ya kuhitimu. Hata hivyo, tokea kubinafsishwa kwa huduma za Hospitali hiyo, kumekuwa na utaratibu mpya usio rafiki kwa wanafunzi wanaokwenda hapo kwa mazoezi ya vitendo kwa sababu ya kubinafsishwa kwa baadhi ya vitengo.

(a) Je, ni upi utaratibu mpya wa wanafunzi wanaokusudia kufanya mazoezi ya vitendo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

(b) Je, ni kiasi gani cha ada kilikuwa kinalipwa kabla ya ubinafsishaji na kiwango gani kinalipwa sasa kwa huduma hiyo kwa wanafunzi.

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kuwa mpango wa wanafunzi wa kufanya mazoezi kwa vitendo unakuwa rafiki na rahisi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

163. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Eneo la uwanja wa Malindi ni miongoni mwa maeneo muhimu sana yanayoaminika kihistoria kuwa, chini ya ardhi ya eneo hilo, kuna uwezekano mkubwa wa kupatikana mabaki ya vitu mbali mbali vya kale.

Je, kuna taarifa zozote za kupatikana vitu vya kale kutokana na uchimbaji unaofanyika hivi sasa wa mradi mkubwa wa kimkakati.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

47. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wanafunzi na walimu wa skuli ya Msingi ya Maziwani katika jimbo la Pandani wanajifunza na kufundisha katika mazingira yasiyoridhisha, huku bati la skuli likiwa linavuja, ofisi ya Mwalimu Mkuu ikiwa haina mlango, watoto takriban 502 wanatumia matundu matatu tu ya vyoo na hakuna mazingira rafiki kwa watoto wenye mahitaji maalumu wala vitendea kazi vya kuridhisha.

(a) Je, ni lini Serikali itaiezeka upya skuli ya msingi ya Maziwani ili isivuje.

(b) Je, ni lini mlango katika ofisi ya Mwalimu Mkuu utawekwa sambamba na kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye mahitaji maalumu.

(c) Je, kwa wanafunzi wasiopungua 502, ni matundu mangapi ya vyoo yanahitajika na lini yataongezwa kutimia idadi hiyo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

28. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetoa boti kwa wavuvi na boti nyengine kwa wakulima wa mwani.

(a) Je, kupitia zoezi hili, ni boti ngapi zimeshatolewa kwa wakulima wa mwani.

(b) Je, kupitia boti hizo ni kiasi gani cha pesa kimetumika.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

120. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na matatizo ya mafunza ya embe kwa muda mrefu sasa na Wizara yako imekuwa ikichukuwa jitihada mbali mbali za kulitafutia ufumbuzi tatizo hili, ingawa mpaka sasa hali bado si mzuri.

(a) Je, Mhe. Waziri unawaeleza nini wananchi wa Zanzibar juu ya tatizo hili.

(b) Je, ni lini wananchi hao wategemee kuondoka kwa tatizo hili.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

73. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu sasa kumejitokeza changamoto ya kupatikana maji safi na salama katika shehia ya Michamvi.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu tatizo hilo.

(b) Ni lini tatizo hilo litatatuliwa ili wananchi hao waweze kupata maji safi na salama.

(c) Ni ipi mikakati ya Serikali kwa wananchi wa vijiji vya Michamvi na vitongoji vyake.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto:**

153. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto:

Wananchi wengi hususan kina mama wamejiingiza katika mfumo wa vikoba kwa ajili ya kujinasua na hali ngumu za maisha.

Je, ni kwa kiasi gani vikundi hivi vimekuwa na matokeo chanya na changamoto gani wananchi wamekuwa wakikumbana nazo mara kwa mara kupitia vikundi kama hivi.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**16 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**